Nafasi ya Hadithi Katika Jamii ya Wameru: Uhakiki wa Hadithi za Waigembe

Tasnifu hii imetolewa kama sehemu mojawapo ya mahitaji ya shahada ya M.A katika Chuo Kikuu cha Egerton.


Na
Muthare C. Karimi


Januari, 1998

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

**YALIYOMO** **UKURASA**

UNGAMO v
TABARUKU vi
SHUKRANI vii
KIINI CHA TASNIFU ix

**SURA YA KWANZA** 1
1.0 UTANGULIZI 1
1.1 SOMO LA UTAFITI 2
1.2 MAELEZO YA ISTILAHI 3
1.3 MAKISIO YA UTAFITI 3
1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI 3
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA 4
1.6 UPEO WA UTAFITI 6
1.7 MISINGI YA NADHARIA 9
1.8 MBINU ZA UTAFITI 12

SURA YA PILI
2.0 UTANGULIZI 15
2.1 HADITHI KATIKA MUKTADHA WA FASIHI SIMULIZI 15
2.2 NAFASI YA HADITHI KATIKA JAMII: MAONI YA WASOMI WA KIAFRIK A 16
2.3 MSANII NA USANII KATIKA HADITHI 22
2.4 MAONI YA WASOMI WA KIMAGHARIBI KUHUSU HADITHI 25
2.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU HADITHI KATIKA JAMII YA WAMERU 30
2.6 HITIMISHO 32

**SURA YA TATU**
**KUSANYIKO NA UCHAMBUZI WA HADITHI**
3.0: KUSANYIKO LA HADITHI 35
3.1: UTANGULIZI 35
3.2: HADITHI ZILIZOTUMIKA 37
3.3: UCHAMBUZI WA HADITHI 98
3.3.1 NDOA NA MALEZI 98
3.3.2 UTANGULIZI 98
3.3.3 MAPENZI NA KUJITOLEA KATIKA NDOA 99



EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

3.3.4 MALEZI YA WATOTO KATIKA NDOA 102
3.3.4.1 MALEZI YA KIMAADILI 109
3..3.4.1.1 UTANGULIZI 109
3..3.3.1.2 UTIIFU 110
3..3.3.1.3 UWAJIBIKAJI 113
3..3.3.1.4 UBINAFSI, WIVU NA ULAFI 117
3..3.3.1.5 MAFUNZO YA KIJUMLA KUHUSU ULIMWENGU 121
3.4 KAZI NA UMUHIMU WAKE KATIKA JAMII 125
3.4.1 UTANGULIZI 125
3.4.2 MAANA YA KAZI 125
3.4.3 MADHARA YA KUTOFANYA KAZI 129
3.4.4 USHIRIKIANO KAZINI 132
3.5 SIASA NA UTAWALA 134
3.5.1 UTANGULIZI 134
3.5.2 UTATUZI WA SHIDA ZA JAMII KWA KUSHIRIKIANA 134
3.5.3 UTATUZI WA SHIDA ZA WATU BINAFSI 137
3.5.4 UONGOZI 140
3.6 HISTORIA, MAZINGIRA NA UTAMADUNI 143
3.6.1 UTANGULIZI 143
3.6.2 HADITHI: HIFADHI YA HISTORIA 144
3.6.3 HADITHI: KUTOA MAFUNZO KUHUSU MAZINGIRA 147
3.6.4 HADITHI: HIFADHI YA UTAMADUNI 151
3.7.0 HITIMISHO LA SEHEMU 155
3.8 NAFASI YA MBINU ZA UTAMBAJI KATIKA KUFANIKISHA UJUMBE 155
3.8.1 UTANGULIZI 155
3.8.2 WAHUSIKA NA UHUSIKA 157
3.8.2.1 WAHUSIKA BINADAMU 158
3.8.2.2 WAHUSIKA WANYAMA 160
3.8.2.3 MHUSIKA ZIMWI 162
3.8.2.4 WAHUSIKA WENGINE 164
3.83 UTENDAJI 167
3.8.4 UCHAGUZI WA MANENO 171
3.8.5 NYIMBO 173
3.8.6 TAKIRIRI 177
3.8.7 TANAKALI ZA SAUTI 180
3.8.8 HITIMISHO 182

## SURA YA NNE


NAFASI YA HADITHI KATIKA JAMII 183

4.0 UTANGULIZI 183

4.1 HADITHI KATIKA MUKTADHA WA KITAMADUNI NA WA KISASA 184

4.1.1 NDOA NA MALEZI 184
4.1.2 MALEZI YA WATOTO 188
4.1.3 WAJIBU WA WATOTO KWA WAZAZI 190
4.1.4 KAZI KATIKA JAMII 191
4.1.4.1 UGAWAJI WA KAZI 192
4.1.4.2 KAZI NA MAZINGIRA 194
4.1.5 SIASA NA UTAWALA 197
4.1.5.1 UCHAGUZI WA VIONGOZI 197
4.1.5.2 UHUSIANO KATI YA FASIHI, SIASA NA DINI 200
4.2 HADITHI: MIKTADHA YA KIUTENDAJI 202
4.2. WAKATI NA MAHALI KATIKA MUKTADHA WA KITAMADUNI 202
4.2.2 UTAMBAJI KATIKA JAMII YA KISASA 204
4.2.3 HADHIRA KATIKA MUKTADHA WA KITAMADUNI 207
4.2.4 HADITHI NA HADHIRA KATIKA JAMII YA KISASA 213
4.3 SWALA LA LUGHA KATIKA MAFUNZO YA FASIHI SIMULIZI 216
4.4 HITIMISHO 220


## SURA YA TANO


5.0 TAMATI 221
5.1 MUKTASARI 221
5.2 HITIMISHO 225
5.3 MAPENDEKEZO 228
MAREJELEO 232

KIAMBATISHO 237

## KIINI CHA TASNIFU

Tasnifu hii imejishughulisha na suala la hadithi katika jamii ya Waigembe, na hasa ikizingatia nafasi ya hadithi hizo katika ujamiishaji. Hadithi zimedhihirisha kuwa na uhusiano wa karibu na utamaduni na mazingira ya jamii husika. Vile vile, imedhihirika kuwa hadithi huwa na majukumu maalum na muhimu ya kutekeleza katika jamii.

Katika sura ya kwanza, msingi ambamo tasnifu hii imejengeka unabainika. Baadhi ya mambo muhimu ambayo yameshughulikiwa katika sura ya kwanza ni pamoja na somo la utafiti, madhumuni na sababu za kuichagua mada, upeo wa tasnifu, mbinu za utafiti, na nadharia ambayo imetumika kuzichambua hadithi katika tasnifu hii.

Katika sura ya pili, maandishi kuhusu hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi yameshughulikiwa. Kuna waandishi wengi sana ambao wameushughulikia utanzu wa hadithi. Baadhi yao wameuangalia utanzu huu katika jamii mahususi, na wengine wameushughulikia kwa kijumla tu bila kurejelea jamii mahususi. Katika kuchunguza maandishi ya wataalam mbalimbali kuhusu hadithi, wasomi wa Kiafrika wameshughulikiwa kwa upana zaidi.

Sura ya tatu ndiyo sura muhimu zaidi katika tasnifu hii. Uchambuzi wa hadithi mbali mbali umedhihirisha kuwa hadithi hutekeleza majukumu maalum katika uelimishaji na ujamiishaji wa wanajamii wa umri na hadhi mbalimbali miongoni mwa Waigembe. Utanzu wa hadithi umedhihirika kwamba hutekeleza wajibu mkubwa wa mawasiliano. Kuhusu mbinu za utambaji, ni dhahiri kuwa

zinachangia pakubwa uelewekaji wa ujumbe unaopitishwa kwa njia ya utambaji. Mbinu zilizoshughulikiwa katika sura hii ni pamoja na utendaji, uchaguzi wa maneno, nyimbo, takiriri, na tanakali-sauti. Utambaji wa hadithi umejitokeza kama sanaa inayowasaidia watoto kuwa wabunifu na kuwa na ujasiri. Waaidha, wanapopewa nafasi ya kutamba hadithi katika vikao vya utambaji, watoto wanapata uzoefu wa kuzungumza hadharani.

Katika sura ya nne, uchambuzi wa hadithi umefanywa kwa undani zaidi kwa kuoanisha mambo yanayojitokeza katika hadithi na yale yanayopatikana katika utamaduni wa jamii iliyozitunga hadithi zenyewe. Imedhihirika kuwa hadithi ni zao la utamaduni wa jamii iliyozitunga na, vilevile, ni sehemu ya utamaduni huo. Kwa hivyo hadithi, kama zao la utamaduni na sehemu ya utamaduni, huwa zinawaelimisha wanajamii kuhusu mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika jamii. Katika sehemu hii pia, mtafiti amejaribu kuonyesha kuwa hadithi hazikuwa muhimu tu katika zama za mababu zetu, bali ni muhimu hata katika jamii zetu leo. Kwa jinsi hii basi, mafunzo yanayopatikana katika hadithi hayajapitwa na wakati.Katika sehemu ya pili ya sura hii, miktadha ya kijamii ambamo hadithi hutambwa imeshughulikiwa, na imebainika kuwa miktadha hii huwa inachangia uelewekaji wa ujumbe katika hadithi.

Kwa jumla, tasnifu hii imejaribu kuonyesha kuwa hadithi ni utanzu ulio na umuhimu mkubwa sana katika jamii, na hautumiwi kuwaelimisha na kuwaburudisha watoto tu, bali unatumiwa na kila mwanajamii.